

Chanzo cha Homa ya Uti wa Mgongo – MenACWY na MPSV4: *Unachohitaji Kujua*

Many Vaccine information Statements are available in Spanish and other languages. See www.immunize.org/vis
 Hojas de información sobre vacunas están disponibles en español y en muchos otros idiomas. Visite www.immunize.org/vis

1 Kwa nini nipokee chanjo?

Ugonjwa wa homa ya uti wa mgongo ni ugonjwa hatari unaosababishwa na bakteria inayoitwa *Neisseria meningitidis*. Inaweza kusababisha homa ya uio wa mgongo (ugonjwa wa mpangilio wa ubongo na uti wa mgongo) na maradhi ya damu. Ugonjwa wa homa ya uti wa mgongo mara nyingi hutokea bila onyo—hata kwa watu wenye afya.

Ugonjwa wa homa ya uti wa mgongo unaweza kusambazwa kutoka mtu mmoja hadi mtu mwingine kupitia mguso wa karibu (kukohoa au kubusu) au mguso wa mbali, hasa kati ya watu wanaoishi katika nyumba moja.

Kuna angalalu aina 12 za *N. meningitidis*, zinazoitwa "makundi ya bakteria." Makundi ya bakteria ya A, B, C, W, na Y husababisha ugonjwa mwingi wa homa ya uti wa mgongo.

Mtu yoyote anaweza kupata ugonjwa wa homa ya uti wa mgongo lakini watu fulani wako katika hatari kubwa, ikiwa ni pamoja na:

- Watoto wachanga chini ya mwaka mmoja
- Vijana na watu wachanga wenye umri wa miaka 16 hadi 23
- Watu wenye hali fulani za kimatibabu zinazoathiri mfumo wa kinga ya mwili
- Wataalamu wa mikrobiolojia wanaofanya kazi na chembechembe za *N. meningitidis*
- Watu walio katika hatari ya janga la kuzuka kwa ugonjwa katika jamii

Hata wakati unatibiwa, ugonjwa wa homa ya uti wa mgongo huua watu 10 hadi 15 walioathiriwa kati ya watu 100. Na kwa wale wanaoponea, takriban watu 10 hadi 20 kati ya kila 100 wataugua ulemavu kama vile kupoteza uwezo wa kusikia, matatizo ya ubongo, matatizo ya figo, kukatwa viungo, matatizo ya mfumo wa neva, au kovu kali kutoka kwa upasuaji wa ngozi.

Chanjo za **homa ya uti wa mgongo ya ACWY** zinaweza kusaidia kuzuia magonjwa ya homa ya uti wa mgongo inayosababishwa na makundi ya bakteria ya A, C, W, na Y. Chanjo tofauti ya homa ya uti wa mgongo inapatikana kusaidia kulinda kutokana na kundi la bakteria B.

2 Chanjo za Homa ya Uti wa Mgongo ACWY

Kuna aina mbili za chanjo za homa ya uti wa mgongo zilizoruhusiwa na Usimamizi wa Chakula na Madawa (FDA) kwa kinga kutokana na makundi ya bakteria A, C, W, na Y: chanjo iliyopatanishwa ya homa ya uti wa mgongo (**MenACWY**) na chanjo ya polisakaraidi ya homa ya uti wa mgongo (**MPSV4**).

Dozi mbili za MenACWY hupendekezwa mara kwa mara kwa vijana wenye umri wa miaka 11 hadi miaka 18: dozi ya kwanza katika umri wa miaka 11 au 12, na dozi ya nyongeza katika umri wa miaka 16. Baadhi ya vijana, pamoja na wenye UKIMWI, wanafaa kupokea dozi za ziada. Muitishe mtoa huduma wako maelezo zaidi.

Zaidi ya chanjo za kawaida kwa vijana, chanjo ya MenACWY pia hupendekezwa kwa makundi fulani ya watu:

- Watu walio hatarini kwa sababu ya kuzuka kwa ugonjwa wa homa ya uti wa mgongo ya makundi ya bakteria ya A, C, W, au Y
- Mtu yoyote ambaye wengu wake umeharibika au umeondolewa
- Mtu yoyote mwenye ugonjwa nadra wa mfumo wa kinga mwilini unaoitwa "upungufu endelevu wa vijenzi saidizi"
- Mtu yoyote anayetumia dawa inayoitwa ecilizumab (pia inaitwa Soliris®)
- Wataalamu wa mikrobiolojia wanaofanya kazi na chembechembe za *N. meningitidis*
- Mtu yoyote anayesafiri kuenda, au anayeishi katika, sehemu ya dunia ambapo ugonjwa wa homa ya uti wa mgongo hutokea mara kwa mara, kama vile sehemu za Afrika.
- Wanafunzi wapya kwenye chuo kikuu wanaishi katika mabweni
- Makurutu wa jeshi la Marekani

Watoto wenye umri kati ya umri wa miezi 2 na 23, na watu walio na hali fulani za kimatibabu wanahitaji dozi kadhaa kwa kinga ya kutosha. Muulizwe mtoa huduma wako wa afya kuhusu idadi na marudio ya dozi, na mahitaji ya dozi za nyongeza.

MenACWY ndiyo chanjo inayopendekezwa kwa watu katika makundi haya wenye umri wa miezi 2 hadi miaka 55, ambao wamepokea MenACWY hapo awali, au wanatarajia kuhitaji dozi nyingi.

MPSV4 inapendekezwa kwa watu wazima wenye umri zaidi ya miaka 55 wanaotarajia kuhitaji dozi moja tu (wasafiri, au wakati wa janga la kuzuka kwa ugonjwa huu katika jamii).



3**Baadhi ya watu hawafai kupokea chanjo hii**

Mjulisha mtu anayekupa chanjo:

- **Ikiwa una mizio yoyote hatari ya kutishia maisha.**

Ikiwa ushawahi kuwa na mzio wa kutishia maisha baada ya dozi ya chanjo ya homa ya uti wa mgongo hapo awali, au ikiwa unapata mzio mkali katika sehemu yoyote ya chanjo hii, hufai kupokea chanjo hiyo. Mtoa huduma wako anaweza kukuambia kuhusu viungo vya chanjo.

- **Ikiwa una mimba au unanyonyesha.**

Hakuna maelezo mengi kuhusu hatari zinazotarajiwa za chanjo hii kwa mwanamke mjanzito au mama anayenyonyesha. Inafaa kutumiwa wakati wa ujauzito wakati inahitajika pekee.

Ikiwa una ugonjwa usio mkali, kama vile homa, kuna uwezekano ukapokea chanjo yako leo. Ikiwa wewe ni mgonjwa kiasi au sana, labda unafaa kusubiri hadi upone. Daktari wako anaweza kukushauri.

4**Hatari za mzio wa chanjo**

Ukitumia dawa zozote, hata chanjo, huwa kuna uwezekano wa madhara. Madhara haya huwa kidogo na hupotea yenyewe baada ya siku chache, lakini mizio hatari pia inawezekana.

Zaidi ya nusu ya watu wanaopokea chanjo ya homa ya uti wa mgongo ya ACWY huwa na **matatizo yasiyo hatari** baada ya kupokea chanjo, kama vile wekundu au maumivu katika sehemu ya sindano. Ikiwa matatizo haya yatatokea, kwa kawaida huisha baada ya siku 1 au 2. Hutokea mara nyingi baada ya kupokea MenACWY kuliko baada ya kupokea MPSV4.

Asilimia ndogo ya watu wanaopokea chanjo huwa na homa kidogo.

Matatizo yanayoweza kutokea baada ya kudungwa chanjo yoyote:

- Wakati mwingine watu huzimia baada ya utaratibu wa matibabu, ikiwa ni pamoja na chanjo. Kuketi au kulala chini kwa takriban dakika 15 kunaweza kusaidia kuzuia kuzirai, na majeraha yanayosababishwa na kuanguka. Mwambie daktari wako ikiwa unahisi kizunguzungu, au kubadilika kwa namna unavyoona au kelele katika masikio.
- Watu wengine hupata maumivu makali mabegani na huwa na ugumu wa kusongeza mkono mahali ambapo sindano ilidungwa. Jambo hili hufanyika mara chache sana.
- Dawa zozote zinaweza kusababisha mzio mkali. Mizio kama hii kutoka kwa chanjo huwa nadra sana, inakadiriwa takriban dozi 1 kati ya dozi milioni moja, na inaweza kutokea ndani ya dakika chache hadi saa chache baada ya chanjo.

Kama tu dawa zozote, kuna nafasi ndogo sana ya chanjo kusababisha majeraha makali au kifo.

Usalama wa chanjo hufuatiliwa wakati wote. Kwa maelezo zaidi, tembelea: www.cdc.gov/vaccinesafety/

5**Na kukiwa na mzio hatari?****Ninafaa kutafuta nini?**

- Tafuta kitu chochote kinachokutia wasiwasi, kama vile dalili za mzio mkali, homa kali sana, au tabia isiyo ya kawaida.

Dalili za mzio mkali zinaweza kujumuisha mabaka ngozini, uvimbe usoni na kwenye koo, ugumu wa kupumua, kasi ya mapigo ya moyo, kizunguzungu, na udhaifu — kwa kawaida ndani ya dakika chache hadi saa chache baada ya chanjo.

Ninafaa kufanya nini?

- Ikiwa unafikiria ni mzio mkali au jambo lingine la dharura ambalo halawezi kusubiri, piga simu kwa 9-1-1 na uende katika hospitali iliyo karibu nawe. La sivyo, mpigie daktari wako simu.
- Baadaye, mzio unafaa kuripotiwa kwa "Mfumo wa Kuripoti Matukio Mabaya ya Chanjo" (VAERS). Daktari wako anafaa kutoa ripoti hii, au unaweza kufanya hivyo mwenyewe kupitia tovuti ya VAERS katika www.vaers.hhs.gov, au kwa kupiga simu kwa **1-800-822-7967**.

VAERS huwa haitoi ushauri wa kimatibabu.

6**Programu ya Fidia ya Majeraha ya Chanjo ya Kitaifa**

Programu ya Fidia ya Majeraha ya Chanjo ya Kitaifa (VICP) ni programu ya shirikisho iliyoungwa kuwafidia watu ambao huenda wakawa wamejeruhiwa na chanjo fulani.

Watu wanaoamini wamejeruhiswa na chanjo wanaweza kupata maelezo kuhusu programu hii na kuhusu namna ya kuripoti madai kwa kupiga simu kwa **1-800-338-2382** au kutembelea tovuti ya VICP katika www.hrsa.gov/vaccinecompensation. Kuna kikomo cha muda wa kuripoti madai ya fidia.

7**Ninaweza kupata maelezo zaidi aje?**

- Muulize mtoa huduma wako wa afya. Anaweza kukupatia kipeperushi cha furushi la chanjo au kupendekeza vyanzo vingine vya maelezo.
- Piga simu kwa idara ya afya iliyo karibu na wewe au ya jimbo.
- Wasiliana na Vituo vya Udhhibiti na Uzuiaji wa Magonjwa (CDC):
 - Piga simu kwa **1-800-232-4636 (1-800-CDC-INFO)** au
 - Tembelea tovuti ya CDC katika www.cdc.gov/vaccines

Vaccine Information Statement
Meningococcal ACWY Vaccines - Kiswahili

03/31/2016

Office Use Only



42 U.S.C. § 300aa-26

Translation provided by Minnesota Department of Health